

# HALMASHAURI YA WILAYA YA BUCHOSA



## MTIHANI WA KWANZA WA UPIMAJI - FEBRUARI 2025 HISTORIA YA TANZANIA NA MAADILI – DARASA LA NNE

Muda: Saa1:30

Mwaka: 2025

### SEHEMU A

**1: Jibu kipengele i-viii kwa kuchagua jibu sahihi kisha uandike herufi yake kwenye paradesi ulizopewa.**

- i. Ulinzi na usalama wa jamii za kitanzania ni jukumu la.....  
A: Wazazi B: Watoto wote C: Wanajamii wote D: Baba peke yake [ ]
- ii. Muunganiko wa familia nyingi zenye asili moja huitwaje?  
A: Familia nyingi B: Wazazi na watoto  
C: Ukoo D: Ndugu na marafiki [ ]
- iii. Ni kundi lipi kati ya haya yafuatayo ndio kitovu cha ukuzaji na utunzaji wa maadili katika jamii?  
A: Wavulana na wasichana B: Watoto na vijana  
C: Watoto na wazee D: Wazazi na walezi [ ]
- iv. Moja kati ya matendo yafuatayo hujenga uhusiano mwema katika jamii zetu za kitanzania.  
A: Kugombana kila wakati B: Kushiriki kwenye misiba na sherehe  
C: Kutengana wakati wa majanga D: Kuhifadhi chakula kingi [ ]
- v. Mchezo wa asili unaochezwa kwa kuchambua mawe yote yaliyo kwenye shimo bila kudondosha huitwaje?  
A: Kuchambua mawe B: Kukimbia  
C: Mdako D: Mchezo wa mashimo [ ]
- vi. Sote tunawajibika kuendeleza mavazi yetu ya asili. Je, ni mavazi gani tunapaswa kuyaepuka?  
A: Mavazi yanayoonisha maungo ya mwili B: Mavazi marefu  
C: Mavazi yanayositiri mwili D: Mavazi yenye rangi nyeusi [ ]
- vii. Mwenendo au utendaji uliokubalika katika jamii huitwa.....  
A: Historia B: Michezo C: Maadili D: Mafunzo [ ]
- viii. Mambo yaliyopigwa marufuku katika jamii fulani kwa mujibu wa imani, utamaduni na desturi zao huitwaje?  
A: Desturi B: Mila C: Nyimbo D: Miiko [ ]

JINA LA MTAHINIWA:..... SHULE.....  
MKOA:..... WILAYA:.....

**2: Jibu vipengele i-vi kwa kuoanisha maneno ya kifungu A na ya kifungu B kisha uandike herufi ya jibu sahihi kwenye kisanduku cha majibu.**

NA	KIFUNGU A	MAJIBU	KIFUNGU B
i.	Ruvuma		A: Jumba lililotumika na sultani
ii.	Bagamoyo		B: Makumbusho ya vita ya Maji Maji
iii.	Kilwa		C: Makumbusho ya Kaole
iv.	Arusha		D: Mji mkuu wa Tanzania
v.	Husuni		E: Makumbusho ya elimu ya viumbe
vi.	Dodoma		F: Magofu ya Ngome ya gereza

### SEHEMU B

**3: Tumia maneno yaliyopo kwenye boksi kujibu vipengele i-vii kwa kujaza nafasi zilizo wazi kwa majibu sahihi.**

TAKUKURU, Kutokubaguliwa, Haki, Katiba, Maendeleo, Kanuni, Wajibu, Upendeleo

- .....ni hali ya ongezeko au kupiga hatua fulani.
- Kupinga vitendo vya rushwa ni.....wa mtoto.
- .....ni haki mojawapo ya mtoto.
- .....huzuia na kupambana na vitendo vya rushwa.
- Sheria na kanuni zinazoainisha jinsi nchi inavyoendeshwa.....
- .....ni mwongozo au taratibu zinazotumika kuelelkeza tabia au shughuli za kundi fulani
- Kitu au huduma anayopaswa mtu kupata ni.....

**4: Chunguza kwa makini picha ifuatayo kisha ujibu vipengele i-iv kwa kuandika majibu sahihi kwenye nafasi zilizo wazi.**



- Ni watu wangapi wanaonekana kwenye picha hapo juu.....
- Je, mtu aliyebeba ndoo anafanya kazi gani?.....
- Taja shughuli mbili zinazofanywa na watu hao;  
a) .....  
b) .....
- Bainisha faida moja ya shughuli inayofanywa na watu hao;  
.....